JIMBO KUU KATOLIKI DAR ES SALAAM.

PAROKIA YA MT. ANNA HANANASIF.

1.HISTORIA FUPI YA PAROKIA.

Parokia ya Hananasif ni mojawapo ya parokia zilizopo katika jimbo kuu la Dar es salaam. Parokia hii ilizaliwa kutoka Parokia ya Mwananyamala.

Mnamo mwaka 1978 kulikuwa na waamini wachache tu katika eneo hili ambao walikuwa wanakusanyika pamoja na katika shule ya msingi Hananasif wakisali pamoja kila siku ya ijumaa saa 10:00 jioni, wakiongozwa na Mapadri wa shirika la Consolata kutoka Parokia ya Mwananyamala.

Ilipofika mwaka 1988, Mapadri hao wa shirika la Consolata waliondoka Parokiani Mwananyamala na nafasi yao kuchukuliwa na Mapadri wa shirika la Jamii ya Maisha ya kitume wa Kazi ya Roho Mtakatifu (ALCP/OSS Apostolic Life Community of Priests in the Opus Spiritus Sancti) chini ya **Padri Plato Tarimo na Padri Thadeus Mshanga. (kwa sasa Padri Plato Tarimo ni marehemu, tunamuombea pumziko la Milele Mbinguni)**

Mwaka huo huo wa 1988 baada ya jitihada kubwa za Mapadri waliokuwepo wakati huo,walifanikiwa kupata jengo lililotumika kama jengo la Kanisa na hatimae kigango. waamini hao walihamia kwenye , jengo hilo chini ya Parokia ya Mwananyamala. Mwishoni mwa mwaka 1988, Padri Tarimo alihamia katika kigango hicho pakiwa pamejengwa nyumba ndogo ya kuishi na kuwa Padri kiongozi.

Padri Plato Tarimo akishirikiana na waamini wachache waliokuwepo wakati huo, alianzisha ujenzi wa nyumba ya mapadri pamoja na kuendeleza maswala mbali mbali ya kiroho na maendeleo ya kigango.

Tarehe 26/07/1993, kigango hicho kilitangazwa rasmi kuwa Parokia na **Padri Plato Tarimo kuwa Paroko wa kwanza akisaidiwa na Padri Antony Mrina.** Mwaka

mmoja baadae, Padri Plato Tarimo aliondoka Parokiani Hananasif na kumuachia utume huo Padri Augustino Shayo.

Waamini waliendelea kuongezeka kadri siku zilivyokuwa zinaongezeka. Mnamo tarehe 02/11/ 2003, Baba Askofu msaidizi Mhashamu Methodius Kilaini, aliweka jiwe la msingi kwa ajili ya upanuzi wa jengo la Kanisa.

Mapadri waliokuwepo wakati huo kwa kushiriana na kamati tendaji iliyokuwepo, waliona ni vyema Parokia ikapata Masista ambao watakuwa wanahudumu hapa Parokiani, hivyo walianza mchakato wa kutafuta kiwanja ili kujenga nyumba ya masista. Baadae walifanikiwa kupata kiwanja nje ya eneo la Parokia na kujenga nyumba ya masista.

Ilipofika tarehe 01/11/2008, Marehemu Muadhama Kardinar Policarp Pengo, aliibariki nyumba hiyo na siku hiyo hiyo waliwasili Masista wa shirika la Maria wa Kakamega kutoka kenya.

Masista hawa wanafanya kazi bega kwa bega na Mapadri katika kutoa huduma hapa Parokiani.

MAPADRI WALIOHUDUMU HAPA PAROKIANI MPAKA SASA

NO	MWAKA	JINA LA PAROKO	JINA LA PAROKO MSAIDIZI1
1	1988	Plato Tarimo	Antony Mrina
2	1994	Pd. Augustino Shayo	Pd. Method Kiwale
3	1998	Pd. Daudi Ndelacho	Pd.Priscus Jumamosi
4	2004	Pd. Gasper Mtengetse	Pd. Thomas Marwa Pd. Very Urrio Mturushwe
5	2017	Pd. Henry Kahumba	
6	2018	Pd. Eladius Kibangura	Pd. Mathew Bura(marehemu) Pd. Peter Nau
7	2021	Pd. Peter Nau	Pd. Lucas Kameku Pd. Apolinary Kibadeni Pd. Thomas Bujiku
8	2025	Pd. Isdor Ndekumanya	Pd. Thomas Bujiku

MAPADRI WAZAWA WA PAROKIA HII MPAKA SASA.

1.Pd Kenedy Lazaro Njau wa shirika la Wafransisco Wakapuchini

2.Pd Henry Damas Kanyau wa Jimbo kuu la Dar es salaam

MASISTA WAZAWA WA PAROKIA HII MPAKA SASA.

1.Sr Hilda Joseph wa shirika la Bikira Maria mama wa yatima

2.Sr Hilda Kimaro wa shirika la Roho Mtakatifu

3.Sr Maria Kavishe wa shirika la Mt. Theresia wa mtoto Yesu

4.Sr. Lucy Kimaro wa shirika la Maria wa Kakamega Kenya

2. UONGOZI WA PAROKIA WA SASA.

(i) Pd. Isdor Ndekumanya	Paroko	0764 797374/ 0784 956771
(ii) Pd. Thomas Bujiku	Paroko msaidizi	0715 060879

KAMATI TENDAJI PAROKIA.

(i)Bw. Emanuel Silvan	Mwenyekiti
(ii)Bi Modester Mushi	Makamu mwenyekiti
(iii) Bi. Felister Sambua	Katibu
(iv)Bw James Bruno	Katibu msaidizi
(v) Bw. Damas Shetui	Mtunza hazina

Mawasiliano ya Parokia. Email - Parokiayamtanna @gmail.com

Mobile - 0766 620811

3. RATIBA ZA HUDUMA.

(i) Misa Takatifu Dominika. Misa ya I - 11:30 Alfajiri

II - 12:30 Asubuhi

III - 02:30 Asubuhi

IV - 04:30 Asubuhi

(ii) Misa Takatifu siku za kazi(jumatatu - jumamosi) 12:30 Asubuhi

(iii) Kuabudu Ekaristi Takatifu. Alhamisi 11:00 Jioni

Ijumaa ya kwanza ya mwezi baada ya misa asubuhi.

(iv) Ubatizo. Kila ijumaa ya mwisho wa mwezi saa 11:00 jioni.

(v) Kitubio. Kila siku kabla na baada ya misa za wiki.

Jumamosi saa 11:00 jioni.

(vi) Huduma kwa wagonjwa wa majumbani - jumatano kuanzia saa 1:30 asubuhi

(vii) Huduma za ofisi - Jumanne, Alhamis, Ijumaa na Jumamosi

Saa 02:30 asubuhi mpaka saa 06:30 mchana.

4. MIRADI YA PAROKIA.

(i) Shamba lililopo kibaha Galagaza, lenye mazao ya nafaka pamoja na matunda

(ii) Nyumba moja ya kuishi eneo la kinondoni shamba.

(iii) Eneo la biashara ambalo linatumika kama gereji.

(iv) Shule ya chekechea. (NB: Bado tunaendelea na taratibu za kukamilisha usajili)